


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI

MKOA WA MBEYA
Simu ya Mdomo: 02590089/2590041
Fax: 025-2590089/2590108
Email. ded.mbarali@mbeya.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 237,
RUJEWANA.

TAARIFA KWA UMMA

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, limepitia na kupitisha mapendekezo ya mpango wa Bajeti kiasi cha **tshs 50,144,125,368.98** kwa mwaka wa fedha **2018/2019** kutoka vyanzo mbalimbali vya Mapato leo tarehe 01/02/2018. Mapato kutoka Serikali Kuu na Wadau wa Maendeleo ni **tshs 45,232,773,368.93** Mapato kutoka vyanzo vya ndani ni **tshs 4,911,352,000.00**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **tshs 33,900,893,000.00** ni Mishahara, **tshs 10,246,289,619.52** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **tshs 5,996,942,749.46** ni matumizi ya kawaida.

Mpango wa Miaka Mitatu na Makisio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha **2018/2019** umeandaliwa kwa kuzingatia, Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya mwaka **2018/2019** uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, Vipaumbele vya Serikali ya awamu ya tano, Maagizo ya Viongozi wa Kitaifa, Mwongozo wa Ruzuku ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu (Local Government Development Grant- LDGD), Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano **2016/2017- 2020/2021**, Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR- TAMISEMI), Mpango Mkakati wa Lishe wa Taifa wa Mwaka **2016/2017- 2020/2021**, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka **2015** na Kanuni zake, Ilani ya Uchaguzi ya **CCM** ya mwaka **2015**, Dira ya Maendeleo ya mwaka **2025**, Mpango wa Maendeleo Endelevu **2030**, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka **2017/2018**, Vipaumbele vya wananchi wa Wilaya ya Mbarali kupitia Mfumo ulioboreshwa wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (*Improved Opportunities and Obstacles to Development- O&OD*)

Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali katika Bajeti yake ya mwaka **2018/2019** itajikita katika Ujenzi/Ukamilishaji wa zahanati katika Vijiji, Ujenzi/Ukamilishaji wa Vituo vya Afya katika Kata, Ujenzi/Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi na Sekondari, Kuwezesha upatikanaji wa Madawati kwa Shule za Msingi na Sekondari, Ujenzi/Ukamilishaji wa matundu ya vyoo katika

Shule za Msingi na Sekondari, Kuboresha miundombinu ya katika Sekta ya Kilimo, Mifugo, Afya na Elimu, Kuboresha Lishe kwa watoto, Ulipaji wa madeni mbalimbali, Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali ili waweze kuboresha bidhaa zao kwa kuwapatia mafunzo ya namna ya kutambulisha bidhaa zao kwa kutumia MsimboMilia (BARCODE), Kuendelea kupambana na Maambukizi ya VVU/UKIMWI, Kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika Uchumi wa Viwanda, Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi (*Climate Change*) pamoja na kutambua jitihada za Jamii katika Kukabiliana na Mabadiliko hayo, Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa kuboresha vyanzo vya mapato vilivyopo pamoja na kubuni vyanzo vipya, Kuboresha miundombinu ya kijamii na kiuchumi hususani katika sekta ya elimu, maji, afya, kilimo, mifugo, uvuvi na barabara kwa kuzingatia ubora wa kitaifa.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali iliidhinisha Matumizi ya kiasi cha **tsh 54,590,921,026.00** kati ya hizo **tshs 51,307,774,026** ni Mapato kutoka Serikali Kuu na wadau wa maendeleo, **tshs 3,283,147,000.00** ni mapato kutoka vyanzo vya ndani. kati ya Fedha hizo, kiasi cha **tshs 28,235,993,800.00** ni mishahara, **tshs 20,784,677,826.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo na **tshs 1,187,102,400** ni Matumizi ya mengineyo. Hadi kufikia **Disemba, 2017** jumla ya **tshs 19,088,296,525.95** zilipokelewa, sawa na **asilimia 35** ya fedha zilizoidhinishwa **2017/2018**.



Daudi B. Nyingo
Afisa Habari
Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali
01/02/2018